## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

**14 MEI, 2018**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_______________

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 14 MEI, 2018

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**230. MHESHIMIWA ALMAS ATHUMAN MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Wilaya ya Uyui inajulikana kwa jina la zamani la *Tabora District Council* (TDC) jina ambalo linagongana na jina la Manispaa ya Tabora *(Tabora Municipality);* Wilaya kupitia Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ilileta maombi ya kubadili jina la Halmashauri kutoka *Tabora District Council* (TDC) na kuwa Halmashauri ya Uyui na Halmashauri imeomba kubadili jina la Jimbo la Tabora Kaskazini na kuwa Jimbo la Uyui ikibeba jina la Wilaya na jina la eneo la kijiografia Uyui kwa sababu hakuna tena Tabora Kaskazini, Kusini wala Magharibi:-

(a) Je, ni lini jina la Halmashauri litabadilishwa kuwa Halmashauri ya Uyui;

(b) Je, ni lini Jimbo la Tabora Kaskazini litaitwa Jimbo la Uyui.

**231. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2014/2015 Jimbo la Magu halikupatiwa Walimu wa Shule za Msingi na bado kuna Uhaba wa walimu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta Walimu Magu.

**232. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Mpwapwa lina Taraja mbili, yaani Tarafa ya Mpwapwa na Tarafa ya Mima, lakini tangu kuanzishwa kwa Tarafa ya Mima hakuna miundombinu yoyote iliyojengwa kama vile Ofisi ya Tarafa na vyumba vya Watumishi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya Afisa Tarafa na za Watendaji wengine ngazi ya Tarafa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)**:

**233. MHESHIMIWA MBAROUK SALIM ALI (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-
Pamoja na jitihada za Serikali katika kutatua kero za Muungano bado kuna manung'uniko mengi kuhusiana na Muungano huu:-

Je, ni kero ngapi mpaka sasa zimeshapatiwa ufumbuzi.

**234. MHESHIMIWA DKT. JASMINE TISEKWA BUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-
Milima ya Uluguru ni chanzo kikubwa sana cha maji katika mito na vijito vingi ambayo husaidia kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa maji safi na salama katika Mkoa wa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam lakini kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na ujenzi holela, kilimo na ufugaji, mito hiyo imeanza kukauka hivyo kusababisha adha kubwa ya upatikanaji wa maji kwa Wananchi:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kimkakati ya kuilinda milima hiyo isiendelee kuharibiwa na kuhakikisha miti iliyokatwa inapandwa mingine ili kuhifadhi vyanzo vya maji.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**235. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Tanzania haijaidhinisha na kujiunga rasmi na Mkataba wa kupambana na Silaha za Sumu (*Biological Weapons Convention)*:-

(a) Je, kwa nini Tanzania haijajiunga na Mkataba huo;

(b) Je, Serikali inafahamu madhara ya kutoidhinisha rasmi Mkataba huo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**236. MHESHIMIWA LUCY SIMON MAGERELI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera

chini ya Kampuni ya Serengeti Limited ulianza Machi, 2013 na Desemba 2016 ulitarajiwa kukamilisha visima 20 ambavyo vitawahudumia Wananchi wa Kigamboni na Mkuranga. Waziri wa Maji na Umwagiliaji Oktoba, 2016 alitembelea Mradi huo na kuagiza ukamilike kwa wakati uliopangwa vinginevyo Kampuni ingelipa gharama za ucheleweshaji, lakini hadi leo mradi huo haujakamilika:-

(a) Je, Serikali imeshaiwajibisha Kampuni hiyo kwa kuchelewesha utekelezaji wa Mradi huo;

(b) Je, ni lini Mradi huo utakamilika ili kuondoa adha kwa Wananchi wa Kigamboni ambao wengi wao wanatumia maji ya visima vifupi ambavyo si salama.

**237. MHESHIMIWA HAROON MULLA PIRMOHAMED (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itamalizia kujenga skimu za Umwagiliaji za Ipatagwa, Kongoro/Mswiswi, Motombaya na Ujenzi wa skimu mpya ya Mhwela mpaka Kilambo pamoja na ujenzi wa

banio la Igumbilo Kata ya Chimala ambalo lilibomolewa na maji mwaka 2016.

**238. MHESHIMIWA MENDRAD LUTENGANO KIGOLA (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Miundombinu ya maji katika Kata ya Igowele, Nyololo, Mninga, Mtambula, Nyigo na Idunda.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**239. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ubakaji na udhalilishaji wa Wanawake na Watoto nchini bado ni tatizo kubwa:-

Je, Serikali inasema nini katika kupambana na Wanaume wanaodhalilisha Wanawake na Watoto.

**WIZARA YA MADINI:**

**240. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali imejipangaje kuwatengea eneo la kuchimba madini katika Mgodi wa Shanta ulioko Mang'onyi (Singida), wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Ikungi na Mkoa wa Singida wanaotegemea kupata kipato kwa shughuli hiyo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **S. KAGAIGAI** |
| **14 MEI, 2018** | **KATIBU WA BUNGE** |